

Ben R. Mtobwa
1994 (1989)
DAR ES SALAAM USIKU
Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

Nacherzählt von
Lourenco Noronha
Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur
am
Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien
Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: Mai 2009

Widmung
Kutabaruku

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

1. Einleitung

1.1. Thematische Einführung

Adili bedeutet „Ethik“, „Moral“ und „gutes Benehmen“. Die Swahili-Literatur der *Maadili*-Gattung beabsichtigte Werte zu tradieren, die der *adili* entsprechen. Zu den Ausläufern der Autoren dieser Gattung gehörte Shaaban Robert (1909-1962). Am 5. Juni 1968 lud der Präsident Tansanias Julius Kambarage Nyerere einige Schriftsteller zu sich und beauftragte sie, durch ihre Texte die *Ujamaa*-Ideologie ins Volk zu tragen. Diese Richtung, genannt *Ujamaa*-Literatur, trat in der zweiten Hälfte der 60er Jahre des vergangenen Jahrhunderts in Erscheinung und hielt an bis in die erste Hälfte der 80er Jahre. Mit der politischen und wirtschaftlichen Liberalisierung, die 1985 einsetzte, änderte sich die Thematik. Die Autoren haben dies erkannt und schrieben das, was sie sehen. Zu solchen Texten gehört der Roman Dar es Salaam Usiku.

Ben Mtobwa, der am 28. August 1958 in der Kigoma-Region, Tansania geboren wurde und Kriminal- und Spionageromane verfasste, schildert in Dar es Salaam Usiku in einer bisher unvorstellbaren derben Sprache einen Aspekt des Lebens in der Hauptstadt Dar-es-Salaam, der mit dem Begriff *matapeli* (S. 63) gekennzeichnet wird. Auf der hinteren Umschlagseite behauptet der Verleger: „*Wahusika ambao ni watu wa tabaka mbalimbali, wanatoa picha halisi ya hali ilivyo jijini Dar es Salaam, mchana na usiku*“. Diese Behauptung ist einseitig. Die Kritik an der Durchführung des *Ujamaa*-Sozialismus, wie sie auf Seite 67 teilweise angedeutet wird, sowie die Hinweise in diesem Roman auf Nebenwirkungen der Liberalisierung sind jedoch ernst zu nehmen.¹

Die zwei Hauptpersonen sind ein älterer Neureicher namens Peterson und ein junges Straßenmädchen Rukia, das er zu seiner Geliebten macht. Eine dritte Hauptperson wird später eingeführt: Hasira, ein ehemaliger Straßenjunge, der mit einer Postkartenfirma ein ansehnliches Vermögen gemacht hat. Er wiederum engagiert einen Straßenjungen Hasara, den er in seine dubiosen Geschäfte einzuführen versucht. Abseits der Haupt- und Nebenpersonen werden Grace, die Sekretärin von Peterson, Rashidi, sein Rechtsberater, Nunu, seine Mutter, Peter, sein Vater, Kautipe, sein Hausdiener und Pambo, eine Zuhälterin eingebaut. Inder und Araber kommen pflichtgemäß in sozialen Rollen vor. Es ist jedoch eine Novität, daß ein europäischer Tourist eingeführt wird. Dieser lässt sich von afrikanischen Prostituierten verwöhnen. Auch ein anderer Europäer wird erwähnt. Die Mutter Rukias, die als Prostituierte in Mwanza arbeitete, verreiste mit einem Europäer nach Nairobi und ließ ihre Tochter allein.

Das Hauptthema ist *matapeli*, ein Begriff, der im neoliberalen Tansania zu einer Verhaltensnorm und einer Lebensweise zu werden droht. Die zwei Nebenhandlungen sind die aufrichtige Beziehung zwischen Rukia und Hasara, die einander nichts zu geben haben außer Liebe und Hoffnung auf ein besseres Leben, sowie die trotz jedes erdenklichen Wohlstands zerrüttete Ehe von Peterson und Gloria. Die Wende Rukias vom Luxusleben bei Peterson zu einem Leben in Armut bei Hasara ist auch bei Bahati im Roman Kiu zu finden.

Es ist eigenartig, dass der Autor Ben Mtobwa andere bekannte Autoren aus Tansania nennt, die sich (angeblich) in der *Bar Tausi* vergnügen. Es sind Hammie Rajab, Kajubi Mukajanga, Nicco Mbajo und John Rutayisingwa (S. 22).

1 “(...) *walikuwa wakizungumza lugha ya aina moja tu, pesa.*” (Uk. 14).

Namen in der Swahili-Literatur haben einen Bezug zur Rolle der Person im Text selbst. Die Neureichen Peter, Peterson, Gloria, Sonny, Happy und Grace tragen Namen, die von Europa und Amerika herkommen. Diese Weltteile werden mit Wohlstand identifiziert. Die Straßenjungen Hasara und Hasira tragen Kiswahili-Namen. *Hasara* bedeutet „Mangel“ und „Verlust (Defizit)“, *hasira* hingegen „Zorn“. Von seiner Mutter erhielt Hasara den Namen Dunia. Der Begriff *dunia* bedeutet „Welt“, wird in Kiswahili-Sprichwörtern manchmal als unberechenbares Schicksal² interpretiert und eher im negativen Sinne verstanden. In diesem Roman scheint „*dunia*“ etwas Rätselhaftes zu besagen. Die Mutter Dunias sagt: „*Dunia imeanza lini kumwelewa kiumbe wake?*“ (uk. 155). In mehreren Aussagen bringt Hasira seinen Zorn und seinen Hass gegen die Neureichen zum Ausdruck. Rukia ist ein bekannter Frauenname und könnte auf das arabische Wort *rooqah*³ zurückgeführt werden. In diesem Fall besagt der Name Rukia „schön“, „hübsch“. Der Name Rashidi ist wiederum arabischen Ursprungs und bedeutet „right minded“, „right guided“, was gut zum Rechtsberater Petersons passt. Die charmante Sekretärin, die liebevoll um Peterson und sein Geld besorgt ist, heißt Grace. Die Zuhälterin, die Nunu ins Bordell bringt, bekommt den bunten Namen Pambo, was „Schmuck“ bedeutet. *Ununu* ist in Kiswahili eine Bastfaser und wird in Zusammenhang mit Palmblättern verwendet. In diesem Roman sind vermutlich Nunu und Kautipe keine Kiswahiliwörter. Ein gewisser Bougwan hilft Peterson gegen Trinkgeld bei seinen zweifelhaften Geschäften. Es gibt einen indischen Name Ba(u)ghwan, der ähnlich klingt. Weder die Araber, noch die europäischen Touristen, noch die Inder haben Eigennamen.

Der Roman wird mit Rückblenden erzählt. Der Aufbau ist straff geordnet, die Personen sind - etwas übertrieben - kontrastweise charakterisiert, ebenso der Gegensatz zwischen Oysterbay und Magomeni, Indiana Hotel und dem Lager der Obdachlosen. Der Schluss jedoch ist sehr schwach, eine unglaublich Schnulze. Es kommen leider zu viele Personen und Nebenhandlungen vor - wie die Suche nach der Mutter -, die vom straffen Ablauf ablenken.

Es kommen Begriffe und Wörter vor, die zu den Neologismen gerechnet werden können.⁴ Die Sprache dieses Romans entspricht den Normen des *Kiswahili Sanifu* (*Standard Kiswahili*). Redewendungen und Sprichwörter gehören wesentlich zur Swahili-Literatur. In Dar es Salaam Usiku trägt der Autor dieser Tradition auch Rechnung. Zu diesen gehören „*Hakuna raha isiyo na karaha*“ (uk.89) und „*Umeonja asali, unataka kuchonga mzinga*“ (uk. 84) und *Hayawi, hayawi, huwa* (uk.150).

Eine Literaturkritikerin aus der Europäischen Union hat diesen Roman als Pornographie

2 *Dunia mwendo wa ngisi, kamwe msiliwale*. Wörtlich: Die Welt bewegt sich wie ein Tintenfisch. Das darf man nie vergessen (übersehen). Auslegung: Diese Welt ist unberechenbar. Wenn man nicht aufpasst, wird man in ihren Fänge geraten.

3 Ahmed, Salahuddin. 1999. A Dictionary of Muslim Names. London: C. Hurst & Co. p. 315.

4 *Tai nyekundu* (uk.6), *gari langu lilipata pancha* (uk.9), *kitita cha noti* (uk.11), *Bustani ya Edeni* (uk.14), *bawa la kuogelea* (uk.16), *glasi* (uk.18), *stage shoo* (uk.24), *msichana wa mapokezi* (uk.28), *nuru ya kibatari* (uk.37), *honi ya treni* (uk.58), *Niliona lebo (labels)* (uk. 63), *check book* (uk.65), *injini ya Benzi* (uk.69), *kanyaga klachi* (uk. 69), *aliweka gia* (uk.69), *akakanyaga breki* (uk.69), *nikupe lifti* (uk.69), *lango la geti* (uk. 96), *mashine ya (kurekebisha) hewa* (uk.70), *pea mbili* (uk.141).

bezeichnet. Es mag so aussehen, der Schwerpunkt jedoch liegt auf dem Hauptthema *matapeli*. Dar es Salaam Usiku sollte in diesem Kontext ausgelegt werden.

1.2. Literaturhinweise

1.2.1. Primärliteratur

Die Zahlen in Klammern beziehen sich auf die Signatur der Fachbibliothek für Afrikawissenschaften und Orientalistik der Universität Wien.

Mtobwa, Ben. 1988 (1984). Pesa zako zinanuka. Dar es Salaam: Heko Publishers/Nairobi: EAEP. 115pp. (B.8.6.6.). (1988. Give me Money. London: Macmillan).

Mtobwa, Ben. 1986. Joram Kiango Mikononi mwa Nunda. Dar es Salaam: Heko Publishers. 97pp.

Mtobwa, Ben. 1989 (1987). Tutarudi na Roho zetu. Dar es Salaam. Heko Publishers/Nairobi: EAEP. 130pp. (B.8.9.102). (Zero Hour. London: Macmillan).

Mtobwa, Ben. 1996 (1987). Salamu kutoka Kuzimu. Dar es Salaam: Heko Publishers/Nairobi: EAEP. 139pp. (B.8.6.306.).

Mtobwa, Ben. 1994 (1990). Dar es Salaam Usiku. Dar es Salaam: Heko Publishers. 153pp. (B.8.6.303.).

Mtobwa, Ben. 1991. Kisa cha Mpaka kupenda Jikoni. Dar es Salaam: Heko Publishers. 32pp.

Mtobwa, Ben. 1996 (1994). Roho ya Paka. Dar es Salaam: Heko Publishers. 159pp. (B.8.6.294.).

Mtobwa, Ben. Nitakusubiri. Dar es Salaam: Heko Publishers. 54pp.

Mtobwa, Ben. 1998. Mpofu mwenye Miwani myeusi (meusi). Dar es Salaam: Heko Publishers. 30pp. (B.8.7.48.).

Mtobwa, Ben. 2000. Mpishi Mwenye Kibiongo. Dar es Salaam: Heko Publishers. 55pp. (B.8.6.357.).

1.2.2. Sekundärliteratur. (*Noch keine gefunden*).

2. Texte
Matini

Rukia betrachtet sich im Spiegel.

(*Rukia*) Alimtazama kwa makini msichana huyo aliyesimama mbele yake katika kioo, akimkabili. Kikiwa kioo chenye zaidi ya urefu wake, aliweza kumtazama tangu miguuni hadi utosini. Akaviusudu vidole vyake vyembamba, akautamani mguu huu laini ambao kwa juu ulibebwa na paja nene jekundu, akaridhika na wingi wa nyama iliyojaa kiungwana nyuma ya mapaja hayo. Kiuno chembamba kilichokatika kama anavyotaka kila mwanamume kikamfanya atabasamu, matiti yaliyoshiha ambayo yalikita kifuani kama yanayukebehi umri kwa kutokuwepo kwa dalili yo yote ya kuusujudia yakamfanya ajipongeze, sura nzuri yenye dalili zote za msichana asiye na hatia ikamfanya achekelee na nywele ndefu laini zilizingira sura hiyo kama bustani nyeusi zikamfanya ajikute akitabasamu. Tabasamu jepesi, tamu, kitu kingine ambacho ni tunu kwani kingeweza kumroga (loga) mwanamume ye yote. (*Uk. 1*).

Sie befindet sich allein im Prachtzimmer eines Luxushotels in Dar-es-Salaam. Ein Mann, den sie auf der Straße kennengelernt hatte, hat sie hierher gebracht, die Nacht mit ihr verbracht, mit Geld versorgt und allein zurückgelassen. Drei Tage sind seither vergangen. Sie ärgert sich.

Ni hilo ambalo lilimfanya Rukia akiacha kitanda laini, na kutupa shuka (Frauenkleid) zote hata akasimama mbele ya kioo hiki, kama alivyozaliwa akijitazama kwa hasira. Pengine ameanza kuzeeka? Uzuri wake unatoweka? Mara hii!, ... Alijiuliza wakati akijitazama. Hasira ambazo zilitoweka baada ya kujitazama sana na kuona tena kuwa yeye bado ni tunu yenye thamani sana machoni mwa wanaume. Pengine bwana huyo ni „jeuri“ au „ana kasoro.“

„Awe jeuri ... awe na kasoro ... hapa ametua,“ Rukia alinong’ona. “Nitamwonyesha kuwa Rukia si mtu wa kurukia ovyo. Jasho linamtoka. Asipojihadhari hata chupi ataiuza ... Awe waziri, awe balozi ...” alisisitiza tena akimtazama msichana huyo ambaye alikuwa akiafikana naye katika kioo. “Ndiyo ... usiku ...,” alifoka kwa mning’ono. (*Uk. 2*).

Sie sinnt nach. Sie war zehn Jahre jung als ihre Mutter, die als Prostituierte in der Stadt Mwanza ihren Lebensunterhalt verdiente, eines Tages nicht mehr nach Hause zurückgekehrt ist.

„Mama yake alikuwa ametoroka kwa mara nyingine. Wala safari hii hakuona kama angeweza kumpata tena, kwani ilisemekana alionekana akipanda basi la Nairobi, akiwa na bwana mpya, Mzungu. (*Uk. 2*).

Rukia war allein. Sie hatte weder eine Wohnung, noch Geld, noch etwas zu essen. Sie besuchte gelegentlich Bars, aber die Männer mieden sie, weil sie ein msichana kind (uk. 2) war. Eines abends kam ein Fremder in die Bar, beobachte sie, hatte Mitleid mit ihr und bestellte ein Abendessen für sie.

Msichana alipowekwa chakula hicho mezani alimtazama mhudumu kwa mshangao. Mhudumu akamwonyesha nani aliyempa chakula hicho. Macho ya msichana huyo

yakakutana na mfadhili wake. Mtu mzima, mwenye tumbo kubwa, mavazi ya gharama na dalili zote za ‚mtumiaji mzuri‘. Msichana huyo akaachia tabasamu. Tabasamu ambalo bwana lilimtia kiwewe. Kwani lilikuwa zuri sana, la kuvutia sana. Hakutegemea. (uk.2).

Sie genießt das Essen nach Tagen des Hungers. Sie möchte ihren Dank zum Ausdruck bringen.

Lilitukia jambo jingine ambalo pia hakulitegemea. Kwani dakika iliyofuata msichana huyo alikuwa tayari ameketi naye meza moja na kuzungumza taratibu, „Sijui nikushukuru vipi.”

Alikuwa akinong’ona. Sauti ilikuwa nzuri vilevile.

„Nenda kale,” alijibiwa.

„Nitakula baadaye,” aliongea taratibu. „Wananiita Rukia ... Sijui mfadhili wangu unaitwa nani?”

„Kale kwanza ...,” alisita kwa mshangao uliompata ghafla.

Mkono wa msichana huyo ulikuwa umetua ghafla juu ya paja na kuanza kulichezea.

„Sikiliza ... ,” alijaribu kufoka.

„Kweli. Niruhusu nikuonyeshe walao shukrani zangu. ...“

Mkono ulikuwa ukipanda. Ulivifikia vigungo vya suruali na kuanza kuvifungua.

Kiza kilichokuwemo kisingetosha kufanya watu waliokuwa meza za mbali kuona kinachotokea. Wachache walitabasamu. Bwana huyu alitayahari. Alimtazama msichana huyo ambaye sasa alikuwa amefika alikotaka kufika na kuanza kuinama huku akisema sasa taratibu, „Niruhusu“. Uso wake mzuri ulikutana na kofi kali ambalo lilimtoka bwana huyo na kutua barabara shavuni mwake. Kofi la pili lilimfanya aanguke na kiti chake. Bwana yule alimtazama kwa dharau, kisha alisema, „Una wazimu,” akainuka na kutoka nje ya baa huku akijilazimisha kutotazama nyuma ambako kila mtu alikuwa akicheka.

Rukia hakutokwa na walao chozi moja. Alijizoaoza, akajifuta vumbi na kisha akatoka taratibu kumfuata huyo bwana. (Uk. 4-5).

+

Ein Straßenjunge sitzt in einem Kaffeehaus, das von wohlhabenden und gut gekleideten Gäste besucht wird. Er aber trägt Kleider, die man in Dar-es-Salaam „Kafaulaya“⁵ nennt. Er kennt weder seine Eltern noch seinen eigenen Namen. Man nennt ihn Hasara. In diesem vornehmen Kaffeehaus wartet er geduldig auf Hasira, der auch ein Straßenjunge war, doch jetzt im Wohlstand lebt.

Hasara gerät außer sich, als Hasira ihn einlädt, in sein Auto einzusteigen. „Woher hat dieser ehemalige Straßenjunge denn ein Auto?“, fragt er sich. Hasira versucht, Hasara in das „Geschäft“ einzuführen.

„Tulianza pamoja Hasara,” Hasira aliendelea kueleza „Siwezi kukuacha.“ Lazima twende sambamba. Ni hiyo tu sababu ambayo imenifanya nikutafute. Iko kazi ndogo nitakayokupa. Kipato chake kitakufurahisha. Baada ya hapo nitakupa njia nyingi

5 „Kafaulaya“ bzw „Amekufa Ulaya“ nennt man Kleiderspenden von Europa, die von den Empfängern auf dem Markt preisgünstig verkauft werden.

ambazo zitakufanya uinuke haraka.”

“Ni kazi ipi hiyo?”

„Usiwe na haraka.“ (Uk. 10).

Hasira kauft neue Kleider für Hasara.

Wakati huo walikuwa wamefikia sanamu ya askari. Katitkati ya njia panda ya barabara ya Azikiwe na Makunganya. Macho yao, ambayo yalizowea sana sanamu hiyo hayakuweza kuiona. Macho ya Hasira yalikuwa yakitazama mbele, lakini ilikuwa dhahiri kuwa alikuwa haoni cho chote bali kazama katika lindi la mawazo. Macho ya Haasira yalikuwa yakifanya *window shopping* na kushangazwa na bei za vitu katika duka lililokuwa kushoto kwao. Shati Shs. 17,200/-, suruali Shs. 18,700/-, saa Shs. 26,300/!

„Tuingie katika duka hili!“ Hasira alisema ghafula.

Waliingia.

„Unalionaje shati hili?“

“Zuri sana!”

“Na ile suruali?”

“Nzuri, lakini bei!”

“Viatu gani vizuri hapa?”

“Hivi hapa, lakini”

Mara Hasira akatoa amri. Mhudumu aliamriwa kuvikusanya vitu vyote hivyo na kumpa Hasara. Hasira alitoa kitita cha noti na kuvilipia bila kuomba walao bei ishushwe. Wakatoka nje ya duka. (Uk. 10-11).

+

Peterson sitzt auf der Couch in seinem Wohnzimmer zusammen mit seiner Frau Gloria, Sohn Sonny und Tochter Happy. Gloria merkt, dass irgendetwas mit ihrem Mann nicht stimmt. Sie macht sich Sorgen.

(Gloria) Alikuwa amekulia katika nyumba ambayo haikuwahi kujua njaa wala ufukara. Akasoma katika shule kubwa za kimataifa ambako walilelewa kama malkia wadogo. Na sasa ameolewa na mume aliyejaliwa, mwenye kila ambacho binadamu anahitaji. Jumba kubwa la ghorofa mbili ambalo mchana lilijaa sauti ya muziki na vishindo vya matumishi wengi wanaoifanyia usafi. Jumba ambalo joto kali la Dar es Salaam halikuweza kupenya kwa ajili ya mashine za kurekebisha hewa ambazo zilikuwa katika kila chumba. Jumba ambalo lilizungukwa na msitu wa maua yanayopandwa kistaarabu na kuyavuta macho ya kila mpita njia. Nje ya jumba hilo kulikuwa na mabwawa mawili ya maji. Moja la kuogelea, la pili walifugwa samaki wa aina mbalimbali. Ndani ya jumba kulikuwa na bwawa jingine la kuogelea, kwa ajili ya baba na mama mwenye nyumba. Magari matatu yenye uhakika; Benzi moja, (Peugeot) 504 na B.M.W.⁶ moja vilikuwa chini katika gereji, tayari kumhudumia baba na mama mwenye nyumba. (Uk. 13).

Gloria braucht nicht arbeiten zu gehen. Sie bleibt daheim bei ihren Kindern.

Watoto wao walikuwa na afya nzuri, akili nzuri, wakisoma katika shule nzuri. Sonny,

⁶ Er besitzt zwar auch ein *Pajero*, aber Autos aus Europa hatten einen höheren Status.

kaka yao alikuwa akifanyiwa mipango ya kwenda kusomea Uingereza. Hivi karibuni angeondoka. Mama mwenye hali kama hiyo asiporidhika wapi angeridhika tena kama si akhera baada ya kifo chake? “Siku hizi una mawazo mengi sana darling. Vipi?” mkewe aliongeza. (Uk. 13).

Petersons Gedanken sind zwar anderswo, er versucht aber irgendwie auf die Frage seiner Frau einzugehen.

„Mawazo! Sina mawazo yo yote,“ alimjibu akiiba jicho la kuitazama tena saa yake. Hatimaye alianza kwenda. Baada ya muda mfupi angeondoka. “Nitawaza nini mpenzi?” aliongea akitabasamu, “Mungu anipe nini zaidi? Mke ninaye. Watoto ninayo. Nyumba ninayo. Gari ninalo. Mungu anipe nini?” aliongeza akiutua mkono wake shingoni mwa mkewe na kumvutia kwake. Nyuso zao zikakaribiana. Akambusu. Mkewe alilipokea busu hilo kwa furaha iliyochanganyika na mshangao. Hakumbuki lini mume wake aliwahi kumusu kwa mara ya mwisho. „Sio hapa ... Watoto watakuja...“ (Uk. 14).

Von seinem Vater, der ein erfolgreicher Geschäftsmann war, hat Peterson ein großes Vermögen geerbt.

Bwana Peter, baba yake (Peterson) alikuwa mtu ambaye aliheshimiwa sana hapa Dar es Salaam na kote nchini. Vile vile alikuwa na marafiki wengi nchi za nje. Kila mara nyumba yao ilikuwa imejaa wageni mbali mbali toka nje weusi kwa weupe ambao walikuwa wakizungumza lugha ya aina moja tu, pesa. Mipango ya pesa ilitawala maongezi na vikao vyao vyote. Mishughuliko yao yote ilikuwa ikihusiana na pesa. (Uk. 14).

Seine Mutter hat Peterson nie gesehen.

Pamoja na starehe zote hizo, lilikuwepo jambo moja ambalo lilikuwa lilimkereketa Peterson. Jambo ambalo lilimjia katika fikira zake changa baada ya kufuatana na rafiki zake majumbani kwao na kuwaona wakifurahi na kucheza na mama zao pia. Yeye hakumjua mama. Alijihisi kama aliyepungukiwa. Kama mtu ambaye amevaa shati bila suruali na kupita mbele ya watu. Usiku mmoja alimkabili baba yake na kumwuliza kwa aibu aibu, „Baba kwa nini mimi sina mama?“

Swali hilo lilimshtua sana baba mtu. Hakulitegemea. Wala hakulipenda. Alijua kuwa iko siku limekuja, lakini hakudhani kuwa ingekuwa mapema kiasi hicho. „Huna mama? Nani anasema huna mama?“ alimwuliza. “Mbona simwoni mama yangu?” (Uk. 15).

Mzee Peter war auf diese Frage nicht gefasst.

Mzee Peter alimvuta mwanae na kumpapasa kichwa. Kwa sauti ya upole alimwambia, „Mwanangu. Kama umeweza kuuliza swali hilo basi naona umeanza kukua. Kama ni hivyo nadhani utakuwa na roho ya kiume kiasi cha kupokea habari mbaya kama hii ambayo nitakuambia leo,“ alisita kidogo. Kisha aliongoza taratibu, “Mama unaye, lakini kwa bahati mbaya alifariki wakati wa uzazi wako.”

Wakati huo kufa hakuwa na maana yo yote katika fikra za Peterson.
Hivyo alisema, “Una maana siwezi kwenda kumwona walao mara moja?”
“Mtu akishakufa haonekani. Huwezi kumwona. Wala usithubutu kumtaja tena katika maongezi yako. Ni nuksi kumtajataja marehemu.“ (Uk. 15).

+

Es ist Nacht in Dar-es-Salaam.

Wapenzi wa starehe kote katika jiji la Dar es Salaam, wazee kwa vijana, walikuwa katika pilikapilika za kujistarehesha. Wanywaji walikuwa tele katika mabaa yasio na idadi yaliyozagaa katika jiji zima na vitongoji vyake. Wapenda muziki walikuwa wakilisakata katika kumbi mbalimbali za starehe. Wapenzi wa sinema walikuwa wakilia na kucheka katika majumba mbalimbali za sinema. Hali kadhalika malaya walikuwa wakijiuzua huko na huko katika mitaa na mabaa wakipishana na majizi na majambazi ambao walikuwa kazini vilevile waliangalia kipi cha kudokoa kipi cha kuiba. (Uk. 16).

Das Hotel Embassy wird besonders von Touristen aufgesucht.

Tuko⁷ Embassy. Moja kati ya zile Hotel kubwa za kisasa ambazo zimejengwa zikiwafikiria watalii peke yao. Tuko katika baa ya *Roof Garden*, juu ya paa la jengo hili. (...) Katikati ya ukumbi huu liko bwawa dogo la kuogelea, lenye maji ya bluu ambayo yametulia kwa namna ya kushawishi mtu avue na kuoga. Macho yameliacha bwawa na kuwatazama wateja wengine kwa wizi. Yumo Mzungu mmoja tu, anayeonekana kubabaishwa sana na wasichana wawili wa kibantu ambao ni wao wanaotoa oda kwa mhudumu, ni yeye anayelipa, wanamcheka⁸. Wanamchezea mapacha. Anacheka. Ameridhika. (Uk.16-17).

Hasara hat einen Tisch für sich und Hasira bestellt. Während er auf ihn wartet, beobachtet er ein schönes junges Mädchen, das allein an einem Tisch nebenan sitzt. Sie lächelt ihn an. Hasara ist verlegen. Er hat kein Geld. Inzwischen ist Hasira gekommen und bespricht heimlich sein Vorhaben. Er möchte Hasara helfen, reich zu werden. Inzwischen ist auch Peterson da. Sie beobachten, wie Peterson das schöne Mädchen hinausbegleitet und in seinem Peugeot 505 mitnimmt. Hasara und Hasira folgen ihnen. Sie kommen in die Bar Tausi. Hasiras Vorhaben nach soll Hasara sich mit dem Mädchen, das Hasira Rukia nennt, anfreunden. Hasara bittet das Mädchen zum Tanz. Peterson und sie stimmen zu. Beim zweiten Tanzlied kommen Hasara und Rukia ins Gespräch.

„Waita nani vile mpenzi?“ Kijana huyo aliuliza. Mikono yake ikiendelea kucheza mabonde na milima ya mgongo na kiuno cha msichana huyu.

“Rukia,” aliong’ona.

“Rukia?”

“Niite Rukia tu,” alinong’ona, “na wewe?”

“Miye wananiita Hasara.”

“Kwa nini Hasara?”

⁷ Es gibt eine Tendenz in der Swahili-Literatur, den Stil der *Fasihi-Simulizi* einzubauen, wonach der Autor gelegentlich den Leser anspricht.

⁸ *Wanamcheka* bedeutet: „Sie lachen ihn aus.“

“Wanajua wao.”

“Kina nani?”

“Ni hadithi ndefu,” akasita kidogo na kisha kuongeza, “Sidhani kama naweza kuishi masaa ishirini na nne yajayo bila ya kuonekana tena. Naweza kukupata wapi kesho mchana?”

“Mbona una haraka hivyo?”

Kimya iliyofuata ndiyo iliyowaashiria kuwa muziki ulikuwa umekatika kitambo. (*Uk. 26-27*).

Rukia kehrt zu Peterson zurück. Hasira kommt langsam zur Sache. Er hat einen lukrativen Auftrag an Hasara zu vergeben.

Hasira alimeza bia yake iliyokuwa mdomoni. “Taratibu Hasara, taratibu”, akamweleza. “Ni jambo la siri sana,” akaipunguza tena sauti yake na kusema “Utakalofanya na yule msichana ni juu yako. Kama utamla mbichi utajua mwenyewe. Na kwa uzoefu wangu naona yeye pia yuko tayari ufanye upendavyo. Sijui una hirizi gani inayofanya hawa viumbe wakupende kiasi hicho.” Hasira alisita tena. “Tunayemtaka ni yule bwana” aliendelea taratibu zaidi. “Tunataka afe. Iwe kifo cha risasi, kifo cha kisu, kifo cha sumu au vinginevyo, afe. Tena iwe wiki hii.” (*Uk. 27*).

Peterson und Rukia fahren zum Hotel Indiana und verbringen dort die Nacht.

„Sikia mpenzi. Leo nataka uwe usiku wa aina yake. Usiku ambao kamwe hautafutika katika damu na fikra zetu. Sawa?“

„Sijakuelewa.“

„Ni hivi. Mie ni mjakazi wako. Na nina miaka zaidi ya kumi sijapata bwana. Mama mwenye nyumba hayupo. Miye kijakazi wako nataka kukushawishi au kukulazimisha mapenzi. Wewe hutaki. Umeelewa?“

Peterson alikuwa bado hajaelewa. Lakini hakuhitaji kuelewa kwani alishtukia mikono ya Rukia ikianza kumvua viatu. Ikamvua soksi. Kisha alichezeachezea vidole vyake vya miguu kwa namna ambayo ilileta njaa ya kiume. Mara ulimi ulianza kunyonya vidole hivyo, mikono ilishughulika na vifungo vya suruali. Suruali ilivuliwa, shati ikafuata. Ulimi ulipaa toka vidole na kulamba kitovu. Uliacha kitovu na kupaa ukichzea matiti, kwaba, masikio na pua yake. (*Uk. 28-29*).

Peterson lässt sich gehen.

Peterson alijikuta taabani. Maumivu ya kupendeza yalikuwa yakimvua taratibu. Kama mgonjwa taabani, alishuhudia vazi lake la mwisho likivuliwa mwilini naye akianguka kitandani chali. Aliposhindwa kusthamili na kujaribu kujitetea kwa vitendo alikuwa akisukumwa tena kulala chali huku sauti yenye mahaba ikimnong’oneza taratibu, “Baba ... tulia tu baba ... acha mtumishi wako nikushughulikie ... leo tu bwanaangu (bwana wangu) ... mama hayupo ... tafadhali “ Ilifika hatua ambayo alishindwa kustahimili. Alitapatapa kama samaki anayekaangwa hai. Sauti ya kilio ilimtoka kwa mnong’ono, “Rukia ... darling ... nikupe nini Rukia ... Ah ...”

Jibu ya Rukia ilikuwa kuongeza jitihada na ujuzi katika harakati zake. Yote ambayo Peterson hakuwahi kuyafikiria, yote ambayo hakuwahi walao kuyaona ndotoni yalikuwa yakitendeka katika mwili wake. Yote! Ustahimilivu ulimwishia. Sasa alilia

kwa sauti. Machozi yakimtoka.

Machozi ya mwanamume, ni faraja pekee ambayo Rukia hupata kuiona duniani. Mwanamume anapolia kwa adhabu pekee anayoitaka, kwake ni zaidi ya gari na nyumba. Ni ushujaa wa aina yake. Ushujaa ambao si kila anayeitwa au kujiti mwanamke anaweza kuupata.

Akimtazama Peterson kwa muda. Kisha, aliyafuta machozi yake kwa titi lake jekundu, lililojaa. Kwa mnong'ono alisema, "Pole mwanangu, pole..." Huku akicheza kimoyoyo. "Pole ... mwanangu, ... mimi ni mama mwema ... nyonya utulie." (Uk. 29).

Hasara ist beauftragt, sich in der Nähe des Hotels zu verstecken und sie (Rukia sowie Peterson) zu beobachten. Er gesellt sich zu den Obdachlosen, die ihr Lager dort aufgeschlagen haben. Die Umgebung ist schmutzig. Trotz der vielen Moskitos und Skorpione muß er durchhalten, denn er wird von Hasira dafür bezahlt.

Am folgenden Tag kehrt Peterson zu seiner Frau zurück. Sie stellt keine Fragen. Er frühstückt, fährt aber diesmal mit seinem BMW ins Büro und läßt seinen Diener den Peugeot 505 und seinen Pajero waschen. Seinen Mercedes hat er seiner Frau zum Einkaufen überlassen. Grace, seine Sekretärin, wartet sehnsüchtig auf ihn.

„Karibu Mzee,“ Katibu Mahsusi wake alimkaribisha. „Hamjambo nyumbani?“ „Wazima kabisa, Grace“ alimjibu akipita kuenda mlango wa ofisi yake. (...) „Bosi, kuna simu nne ambazo nadhani ungehitaji kuzijibu,“ alieleza. „Toka wapi na wapi?“ „Moja ni yule bwana wa wizarani. Amesema umpigie. Ya pili imetoka Marekani, ile kampuni ambayo inataka uiwakilisha hapa nchini. Watakupigia baadaye. Halafu walipiga watu wa Kodi ya Mapato. Nimewaambia uko safari. Mwingine ni yule bwana wa kampuni ya Lulu Enterprises. Vile vile atapiga baadaye.“ (Uk. 41).

Peterson ist am Geschäft mit der Firma Lulu Enterprises interessiert.

Simu hii ya mwisho ilimvutia Peterson zaidi. Hawa watu wa kampuni hii walikuwa na mpango wa biashara ambayo kama ingefanikiwa ingemwachia faida ambayo hajapata kuiona tangu alipoanzisha *Continental Distribution Ltd.* Hata hivyo alikuwa hajui kitu kipi kilimfanya asite kufanya nao biashara moja kwa moja na badala yake akiwachelewesha kuwapa jibu linalostahili. (Uk. 41).

Er läßt seinen Juristen Rashidi die Unterlagen der Firma überprüfen. Grace, die schon fünf Jahre für ihn arbeitet, ist sehr effizient.

Huu mwaka wa tano yuko na msichana huyu, lakini hadi leo Grace hajachoka kumtongoza, kwa macho na miondoko yake. „Wanawake siku hizi!“, aliwaza. Kila mwanamume awe mume! Grace pamoja na kazi hii nzuri, isiyo na jasho, yenye mshahara mnono na marupurupu ya kuvutia, na ana mume, bado anataka nini kwake? Kuna wakati ambao Peterson alielekea kupatikana. Wakati huo alifikia hatua ya kuyashika hayo matako na kumbusu, siku walipobaki peke yao ofisini. Jambo ambalo lilimfanya Grace aongeze vituko; kukaa ovyo huku akivaa nguo fupi zaidi, kujichelewesha ofisini na kadhalika. Lakini Peterson hakukubali kupotoka. (Uk. 42).

Heute hat er es besonders eilig. Er möchte für Rukia ein Geschenk kaufen.

Kituo chake cha kwanza kilikuwa kwa sonara wa Kihindi ambaye aliaminka sana mjini.

„Patel,“ aliita. „Nataka kazi ya haraka sana na uhakika.“

„Bila tabu, bana,“ Patel alijibu kwa Kiswahili cha Kihindi, „Hapa iko express. Wee topata bila taabu. Iko taka nini?“⁹

Peterson alichungulia katika kabati la sampuli za mapambo mbalimbali ya kinamama. „Nataka hereni (helini) kama zile palee, pete kama ilee, mikufu ya aina hii miwili, vipuli hivi hapa, bangili kumi na mbili za aina hii hapa na kidani hiki.“ „Sawa bana kubwa“ Patel alijibu akitetemeka. „Bei gani itakuwa?“ „Kwa mtu mwingine nafanya laki sita. Wewe bana kubwa tofanya laki tano elfu hamsini. Sawa?“ „Sawa nikupe cheki au keshi?“ „Kash bana.“ Patel alikuwa akitetemeka waziwazi sasa. „Nitakuletea baadaye.“ Peterson alieleza baada ya kuitazama saa yake. „Nataka vitu hivyo haraka. Naweza kupata lini?“ „Siku tatu baada ...“ „Leo!“ alifoka. „Nataka leo jioni viwe tayari sawa?“ (Uk. 43).

+

Peterson hatte in England ein Gymnasium besucht. Danach studierte er in den USA, mußte aber das Studium wegen der Krankheit seines Vaters abbrechen und kehrte nach Dar-es-Salaam zurück.

+

Peterson übergibt Rukia den Goldschmuck.

Alipoletwa zawadi hizo, usiku wa jana, alikuwa amezipokea kwa mshangao zaidi ya furaha, huku akijifanya amefurahi kupindukia. Alimbusu Peterson mara nyingi na kuzibusu zawadi hizo kama mwenye wazimu. Peterson aliridhika sana na shukrani hizo. Lakini Rukia alijua fika kuwa alikuwa akimtenda unafiki. Roho yake ilikuwa haijasikia lo lote kwa zawadi hiyo. Badala yake alikuwa akijisikia kama yule kuku mwenye njaa aliyepewa kipande cha almasi.¹⁰ (Uk. 48).

Rukia bekommt einen Anruf von der Rezeption. Sie hat Besuch. Hasara ist da. Sie kennt ihn und seinen Namen noch und freut sich sehr, ihn wiederzusehen, denn sie fühlt sich im Herzen ihm näher als Peterson, dem sie Liebe nur vortäuscht. Sie verbringen einige schöne Stunden zusammen. Hasara, der sie als Lockvogel verwenden sollte, vergißt Hasiras Auftrag.

Eines Tages stellt Hasira Hasara zur Rede.

„Umefika wapi?“

„Nini?“

„Umefika wapi katika jukumu ulilopewa (ulilolipewa)?“

„Jukumu lipi?“

9 Die Swahili-Literatur spricht den Indern in Ostafrika die Kompetenz ein genaues Kiswahili zu sprechen ab. Siehe das Stichwort „Soziolect Kibanyani“ am Link [Einführung in die Swahili-Literatur: Prae-Uhuru Literatur](#) auf der Website www.swahili-literatur.at

10 Sprichwort

„Jukumu lipi?“

„Jukumu lipi?“ alishangaa Hasira.

„Umeniambia umekesha juzi pale nilipokuacha. Na umesema usiku wa jana nusura ukeshe. Mara hii hufahamu kuwa unakesha kwa nini?“

Na hapo Hasira alipokumbuka, alitakiwa kuuu mtu. Akajitahidi kumweleza Hasira kuwa alikuwa hajapata nafasi nzuri ya walao kuingia chumbani humo na kumwona mtu mwenyewe.

“Leo mchana nategemea kwenda na kumwona msichana huyo. Kisha nitapanga mkakati.” Alilaghai. (*Uk. 56*).

Peterson kommt nach einigen Tagen zu seiner Ehefrau Gloria zurück. Sie denkt daran, ihn zu ohrfeigen, schweigt aber in der Hoffnung, daß er wieder zu ihr zurückkehrt. Sie nimmt ihn ins Bett. Er bleibt kalt. Sie weint.

Peterson kommt etwas verspätet ins Büro. Grace macht sich Sorgen, weil er seine Dienstpflichten vernachlässigt. Sie macht ihn wieder auf das große Geschäft mit der Firma Lulu Enterprises aufmerksam.

Lulu Enterprises! Peterson aliwaza. Vipi wameweka na moto wa kibiashara kiasi hiki watu ambao wanadai na kuonekana wafanyabiashara waliokomaa? Zaidi kwa nini wanahangaika wakati bidhaa walionayo ni zaidi ya dhahabu katika nchi hii? Makontaina mawili ya tani ishirini na tano kila moja, yakiwa yamejaa aina mbali mbali ya madawa yanayohitajika sana hapa nchini, si zaidi ya dhahabu? Hasa ukizingatia kuwa tayari madawa hayo yako bandarini, yanachotakiwa ni taratibu za kuyachukulia tu na kisha kuyauza. (*Uk. 61*).

Peterson hat Freunde im Ministerium für Gesundheit und auch beim Zollamt. Vorsichtshalber hatte er seinen Juristen Rashidi beauftragt, das Angebot zu überprüfen. Rashidi kommt herein und übergibt ihm ein Dossier mit den Ergebnissen seiner Untersuchung. Peterson ist überrascht.

„Na hii nini? Ni ya kweli haya Rashidi? Wakurugenzi wote watatu wa kampuni hii ni mtu yule yule ambaye anatomia hila ya kubadili sahihi? Na hapa? Hawana ofisi? Iliyoandikwa katika hati yao ni uongo mtupu? Peterson akalitua faili na kumtazama Rashidi usoni. “Mbona sikuelewi Rashidi?”

Unataka kusema nini?“ Aliuliza.

“Kitu gani huelewi, Mzee?”

“Yaani? ... Unachotaka kusema ni kwamba ... kampuni hii ya Lulu ni ... ni ...”

“Matapeli,” Rashidi alimaliza.

„Matapeli! ... Yaani. ...“

„Yaani walitaka kukutapeli. Hawana nini wala nini. Hata kampuni hawana isipokuwa chombo tu cha kubamiza watu. Wewe umeponea chupu chupu. Ungewapa hiyo milioni ishirini usingewaona tena hadi peponi au jehanamu.”

Peterson aliduwaa.

„Nimeenda hata banadarini,“ Rashidi aliongeza. “Nimehonga ili nikague mali zo zote zilizipo hapo kusubiri kuchukuliwa. Hakuna mzigo wo wote wa watu wanaoitwa Lulu.”

“Lakini mbona niliyaaona makontina hayo kwa macho yangu?” Peterson aliuliza. Niliona lebo zote. Zaidi wana hati zote mikononi.”

“Hati za bandia,” Rashidi aliongeza. „Mipango yote ilikuwa madhubuti na tayari kwa ajili ya kukutia ndani.” (*Uk. 63*).

Peterson bricht jeglichen Kontakt mit den Lulu Enterprises ab. Von seinem Vater hatte Peterson die Geschäftspraktiken in Dar-es-Salaam kennen gelernt. Er musste bald zur Kenntnis nehmen, dass sein Wirtschaftstudium im Ausland hier in Dar-es-Salaam nicht zu verwerten war. Die Devise lautet in Dar-es-Salaam: „Kula na watu.“¹¹ (Uk. 66).

Haikumchukua muda kuelewa kinachotukia. Wala hakuwa mzito wa kubadili mkondo wa maisha aliyoyazowea. Mara moja akanza kuishi kama walivyokuwa wakiishi wengine. Kula na watu. Akiwa mtu aliyesoma muda mrefu, mtoto wa mtu maarufu, hakupata shida yo yote kujiingiza katikati ya duara la watu waliokuwa wamezunguka mti wa neema. Akaanza kula matunda, huku akiwa kivulini. Ingawa kazi maalum ya kampuni yake ilikuwa kuuza bidhaa nje, ilikuwa jambo la kawaida kabisa kuona mkono mmoja wa kampuni ukishughukikia ujenzi wa barabara mpya, mmoja ukiuza madawa viwandani, mmoja ukilisha kikosi fulani cha jeshi, mmoja ukiiuzia wizara silaha, mmoja ukiiwakilisha kampuni fulani ya nje n.k. Mikono yake haikuwa na idadi na idadi. Na yote ilifanya kazi za kupendeza. (Uk. 66-67).

Peterson hat Politik nie gemocht. Er hat aber jetzt erkannt, dass er die Politiker für seine Geschäfte braucht, bzw. die Politiker sein Geld brauchen.

Pilika pilika hizo zilimfanya Peterson ajifunze kitu cha ziada, siasa. Tangu masomoni alikuwa amejibidisha sana kuepuka siasa. Hivyo ilikuwa baada ya kuona kuwa siasa, kama dini ni vitu ambavyo daima vilihitaji sana kumeza muda na uhuru wa watu. Yeye alihitaji muda na uhuru wake. Hivyo aliogopa sana kujihusisha na lolote ambalo lingeweza kumfanya apewe madaraka ya kisiasa hasa akizingatia kiwango cha elimu yake na jinsi watu wa aina yake walivyokuwa wanahitajika tangu Azimio la Arusha lilipotangazwa na kuwakimbiza wasomi wengi. Hivyo aliufyata ulimi wake na kujichimbia kama kobe katika gamba lake, asisikike wala hakufikirika. Lakini sasa, baada ya kufumbuka macho aliona wazi kuwa hakuhitaji kuwa mwanasiasa ili kuiongoza nchi. Siasa ni maneno tu. Ni vitendo vinavyohitajika.

Wanasiasa wanaongoza nchi. Lakini ni wenye pesa wanaoitawala.

Maneno yote ya wanasiasa jukwaani aligundua kuwa ni unafiki na mahubiri yasiyo na ukweli. Walisema hili mchana, usiku wakitenda hili. (Uk. 67).

Peterson kauft ein Haus für Rukia im Nobelviertel Oysterbay. Er stellt einen Koch, einen Hausdiener und einen Wächter an. Er kauft ein Auto für sie und lehrt sie Autofahren. Er lässt sie allein, was sie später veranlaßt zu denken: „Hakuna raha isiyo na karaha“¹² (uk.89). Sie braucht noch Petersons Geld, liebt ihn aber nicht.

Hasira besucht Hasara in seiner Slumwohnung und rügt ihn, weil er Peterson noch nicht ermordet hat. Hasira hatte vor, die Bezahlung für die Container von Peterson in Empfang zu nehmen und ihn sofort darauf umzubringen. Er bringt seinen Haß gegen die Neureichen oft zum Ausdruck.

11 Wie soll man diese Devise übersetzen? Ich schlage vor: „Friss, was Du fressen kannst.“ „Kassiere was du kassieren kannst!“ oder: „Tu das, was ohnehin alle tun!“

12 Sprichwort: Hakuna raha isiyo na karaha. *There is no joy without disgust. Intentional meaning: There are no roses without thorns. We have to reckon with ups and downs in life.*

„Unajua sisi wote ni watumwa tu wa watu wachache sana, usiku na mchana tunavuja jasho na kumwaga damu zetu ili kuwaneemesha wao, watoto wao na hawara zao?“

„Akina nani hao?“ Hasira hakujibu.

Baadala yake alizidi kumtolea Hasara jicho la chuki.

“Wewe ni punda tu ambaye amezaliwa kwa ajili ya kuwatumikia wengine. Hujui kama wewe ni kasuku tu uliyeumbwa ili kuwastarehesha wengine. Hapo ulipo una nini cha thamani? Una raha gani ya kuishi duniani? Tazama unavyolala kwa dhiki kuliko hata mbwa wao,” alisita kwa muda. ... “Wao wanafanya kila kitu. Wanapeana mikopo kwa mamilioni; mikopo ambayo hailipwi. Wanapeana mbinu za kuibia serikali na mashirika yake usiku na mchana; mbinu ambazo haziingiliwi. Wanapeana matibabu ya maana, siye tunakufa kama mifugo. Wanapeana vibali vyote vya biashara za maana; siye tunaishi kwa vibarua wao.” (Uk. 78-79).

Hasira gibt zu, daß sein Vorhaben diesmal fehlgeschlagen ist. Hasara braucht Peterson nicht zu töten. Es lohnt sich nicht mehr. Hasira steigt in sein Auto, verabschiedet sich, fährt ab und läßt sich nie mehr sehen. Die Nachbarn staunen, daß jemand mit einem teuren Auto Hasara besucht hat und vermuten, daß er dunkle Geschäfte macht.

Hasara wäscht sich, zieht seine besten Kleider an und geht auf die Suche nach Rukia. Er besucht das Indiana Hotel. Die Frau an der Rezeption, die ihn kennt, empfängt ihn freundlich aber spöttisch. Er weicht ihren vielen Fragen aus und begrüßt sie.

„Hujambo lakini, shangazi?“

„Miye mzima. Hofu kwako tu“, alijibiwa. ...

Alikuwa mzuri. Lakini uzuri wake ulikuwa ule wa kununua madukani. Uzuri ambao ulitegemea sana pesa. Huo ndio ulimfanya awe na nywele hizi za singa, ngozi nyekundu inayomeremeta, midomo ya rangi na mavazi ya gharama ambayo kwa vyo vyote yangemfanya mwanamke ye yote apendeze. Hasara kamwe hakubabaishwa na wazuri wa aini hii.

„Huyo Rukia mbona unamtafuta sana mwenzetu?“ msichana huyo aliongoza baada ya kuona Hasara kamsahau tena.

„Inaelekea umemshiba kupita kiasi.“

„Labda“ Hasara alimjibu.

„Lakini hasa ambacho nahitaji kutoka kwako ni kumwona tu.“

„Kumwona tu?“ alimkebehi „Kumwona tu! Wakati uso wako unaonekana kabisa kuwa una msiba mkubwa kwa kutokumwona! Mimi nadhani huyo dada alikuonjesha asali ya aina yake, sasa unataka kuchonga mzinga¹³.“ Alimaliza kwa kuachia kicheko laini. „Hata hivyo nadhani umechelewa kidogo“, aliongeza baada ya kumwona Hasara kimya. “Wenzako wamekwisha chonga mizinga (...)” akacheka tena. „Yule mwenzetu sijui amepata mganga gani. Ningemjua mimi ningempa hata roho yangu ili na miye niipate hiyo hirizi.“ (Uk. 83-84).

Sie macht sich lustig über Hasara, erklärt ihm, daß Rukia für ihn nicht zu haben sei, und bietet sich selbst zum Spaß als Ersatz an. Sie fragt nach seiner Wohnanschrift. Er antwortet nicht und dreht sich um. Sie ruft spöttisch: „Mbona unaondoka bila kuniaga,

13 Sprichwort: *Anayeonja asali, huchonga mzinga*. He who tastes honey, craves out the beehive. Intentional meaning: If you find access to something you longed for, but could not get it, you will then probably find it difficult to observe the proper limit.

